



Mwenye kusimama usiku wenyе cheo (Lailatul Qadri) kwa imani na kutaraji malipo, husamehewa madhambi yake yaliyotangulia

Imepokewa Kutoka kwa Abuu Huraira -Radhi za Allah ziwe juu yake- amesema:
Amesema Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake-: "Mwenye kusimama usiku wenyе cheo (Lailatul Qadri) kwa imani na kutaraji malipo, husamehewa madhambi yake yaliyotangulia."

[Sahih] [Wamekubaliana Bukhaariy na Muslim]

Anaeleza Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- kuhusu fadhila za kusimama usiku wa cheo unaokuwa katika siku kumi za mwisho wa Ramadhani, nakuwa yeyote mwenye kujitahidi ndani yake kwa ibada ya swala na dua na kusoma Qur'ani na kumtaja Allah, akiwa na imani na hayo, na kwa fadhila zilizoleenza kwayo, akitaraji kwa amali yake malipo ya Allah Mtukufu, si kwa kutaka kuonekana na kusikika, basi husamehewa yaliyotangulia katika madhambi yake.

<https://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/4202>

